
# *Ee Bwana, utuonyeshe wema wako*

**Zaburi 84 9a10, 11, 12, 13 14**

*By: Gloire Vincent*







1. Nisikie anayosema Bwana Mungu:
   hakika, anawaambia watu wake amani.
   Wokovu wake ni karibu nao wenyekumheshimu,
   utukufu wake utakaa katika nchi yetu.

2. Wema na uaminifu zitakutana,
   haki na amani zitabusana;
   katika nchi uaminifu utaota,
   na haki itashuka toka mbinguni.

3. Naye Bwana atatoa yaliyo mema,
   na nchi yetu itazaa matunda yake;
   haki itatangulia mbele yake,
   wokovu utafuata nyayo zake.